

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA KUMI NA TANO

KIKAO CHA AROBAINI NA SITA

12 JUNI, 2024



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA KUMI NA TANO

KIKAO CHA AROBAINI NA SITA TAREHE 12 JUNI, 2024

I. DUA:

II. MASWALI:

OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

592. MHESHIMIWA JULIANA DANIEL SHONZA (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, kuna mkakati gani kumaliza tatizo la uhaba wa Walimu wa kike katika Shule za Msingi na Walimu wa Sayansi Shule za Sekondari Mkoani Songwe.

593. MHESHIMIWA KASALALI EMMANUEL MAGENI (SUMVE):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itajenga Shule ya Sekondari Kata ya Malya Kitongoji cha Mwashilibwa ili kuongeza huduma Vijiji vya Mwitemba, Talaga na Kitunga.

594. MHESHIMIWA VICENT PAUL MBOGO (NKASI KUSINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itasawazisha vilima vilivyopo kwenye Barabara ya Ninde, Kala na Wampembe ambavyo vimekuwa vyanzo vya ajali.

595. MHESHIMIWA BONIPHACE NYANGINDU BUTONDO (KISHAPU):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itajenga Vituo vya Afya Tarafa ya Negezi ili kuboresha huduma za afya kwani Tarafa hiyo ina Kituo kimoja cha Afya.

596. MHESHIMIWA MASACHE NJELU KASAKA (LUPA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini ahadi ya ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ya Chunya itaanza kutekelezwa.

OFISI YA RAIS (UTUMISHI NA UTAWALA BORA):

597. MHESHIMIWA ISSA JUMANNE MTEMVU (KIBAMBA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Utumishi na Utawala Bora):-

Je, hadi sasa Serikali ina madeni kiasi gani ya Watumishi wa Umma yanayohusu likizo, uhamisho na kusafirisha mizigo baada ya kustaafu.

WIZARA YA NISHATI:

598. MHESHIMIWA ASKOFU JOSEPHAT MATHIAS GWAJIMA (KAWE):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:-

Je, lini Serikali itakuja na mkakati wa kutumia Gesi Asilia kuendesha magari nchini ili kuokoa fedha za kigeni zinazotumika kuagiza mafuta nje ya nchi.

WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:

599. MHESHIMIWA INNOCENT SEBBA BILAKWATE (KYERWA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga Chuo cha VETA Wilayani Kyerwa.

WIZARA YA KILIMO:

600. MHESHIMIWA AGNES ELIAS HOKORORO (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, lini Kongani za Korosho za Maranje Nanyamba zitajengwa ikiwa ni ahadi ya Mheshimiwa Rais alipotembelea Mkoa wa Mtwara.

601. MHESHIMIWA REHEMA JUMA MIGILLA (ULYANKULU):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, lini Serikali itaanza kutekeleza Mradi wa Ujenzi wa Bwawa katika Kijiji cha Ichemba.

WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

**602. MHESHIMIWA FRANCIS ISACK MTINGA
(IRAMBA MASHARIKI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, lini Serikali itakamilisha ujenzi wa Kituo cha Polisi Nduguti kwani ujenzi wake umesimama kwa muda mrefu sasa.

WIZARA YA MAJI:

**603. MHESHIMIWA BUPE NELSON MWAKANG'ATA
(VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, lini Serikali itakamilisha mradi wa maji uliopo Mpasa King'ombe Kata ya Kala Wilayani Nkasi.

**604. MHESHIMIWA DKT. JOHN DANIELSON
PALLANGYO (ARUMERU MASHARIKI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, lini Serikali itatenga fedha kumalizia usambazaji wa maji safi na salama Kata ya King'ori Wilayani Meru hususani katika Vijiji vya Meru kwa Philipo.

WIZARA YA MALIASILI NA UTALII:

605. MHESHIMIWA ORAN MANASE NJEZA (MBEYA VIJIJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii:-

Je, lini Serikali itamaliza mgogoro wa muda mrefu wa ardhi kati ya TANAPA Kitulo/TFS na Wananchi wa Kata za Ilungu, Igoma na Inyala.

**DODOMA
12 JUNI, 2024**

**N.J. MWIHAMBI, *ndc*
KATIBU WA BUNGE**

